TANGAZO LA SERIKALI Na. 505 la tarehe 21/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153 (1))*

SHERIA NDOGO YA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa;

Sura ya 331

"chanzo cha maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kizimba cha taka" maana yake ni kizimba cha taka au chombo maalumu kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya jamii kuhifadhia taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala kuu lililoidhinishwa;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"maji taka" maana yake ni mchanganyiko wa kinyesi, mkojo na suluji na taka zenye asili ya kimiminika kutoka majumbani, katika shughuli za taasisi, biashara na viwanda;

"taka" maana yake ni kitu chochote katika hali ya kimiminika, yabisi au gesi ambacho kinatiririshwa, kinatolewa au kuwekwa katika mazingira kwa kiwango au namna ambayo inaweza kusababisha mazingira kubadilika;

"taka ngumu" maana yake ni kitu kisicho katika hali ya kimiminika, ambacho kinatokana na shughuli za nyumbani, mtaani, biashara, viwanda au kilimo.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

**4**.-(1) Kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;

(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;

(c) anachimba shimo la kutupa taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi tatu na upana usiopungua futi mbili;

(d) ana choo imara cha kudumu kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati, tembe, majani au vigae, chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono; na

(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi.

(2) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa.

Uhifadhi wa maji taka

**5**.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka;

(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka chooni, bafuni, karoni au kiwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

**6**. Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa-

(a) kuzingatia masharti na kanuni za afya; na

(b) kuwa na kibali kutoka kwa afisa afya wa Halamshauri.

Upimaji wa afya

**7**. Mhudumu wa hoteli, mgahawa, baa, nyumba ya kulala wageni, bucha, muoka mikate au mtu anayeshughulika na kuuza vyakula vilivyopikwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anapima afya yake kila baada ya miezi sita.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**8**.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika eneo lolote la Halmashauri wakati wa muda wa kazi kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

Vifaa vya kuhifadhi taka ngumu

**9**.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi au mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanya

biashara katika eneo lolote la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia taka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya taka hizo kwenye kizimba cha kuzolea taka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyo katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanyia taka ngumu katika eneo lake.

Ada ya uzoaji taka

**10**. Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya taka vilivyoainishwa katika kila kata, na wazalishaji taka watalipia ada au ushuru wa ukusanyaji wa taka kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji taka ngumu

**11**.-(1) Mtu hataruhusiwa kuweka uchafu wenye asili ya majimaji kwenye pipa la taka au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye mapipa ya taka zitabaki kuwa katika milki ya mkazi au mmliki wa eneo hadi taka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na Wakala kutoka katika eneo lake.

(3) Mtu hataruhusiwa kuchoma au kufukia taka ngumu bila kibali cha Halmashauri.

Eneo la kutupa taka

**12**. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalumu kwa ajili ya kutupa taka;
(b) kuweka vyombo maalumu vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

Siku ya usafi

**13**.-(1) Kila Alhamisi ya wiki na Jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na umma.

(2) Kila mkazi wa Halmashauri atakuwa na wajibu wa kushiriki usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika eneo lake na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha eneo la makazi yake, eneo analofanyia biashara, eneo la wazi lililo karibu naye na eneo linalomzunguka kwa umbali wa mita kumi ni safi.

Vikundi vya usafi

**14**. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Makosa

**15**. Mtu anatenda kosa ikiwa-

(a) anaendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;

(b) anafanyabiashara yeyote au kupanga bidhaa nje ya jengo lake la biashara, barabarani, vichochoroni au katika eneo lolote ambalo halikuidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(c) anaruhusu mifugo kuzurura ovyo mitaani au barabarani;

(d) anatupa taka za aina yoyote barabarani au eneo lolote la wazi, kwenye vichochoro au kwenye chanzo chochote cha maji au katika eneo lolote ambalo halikutengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(e) anadondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ambapo gari hilo linapita;

Sura ya 191

(f) anaanzisha shughuli za kiwanda au mradi wowote unaoweza kuathiri mazingira bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(g) anazuia maji kupita njia yake ya asili kwa kujenga, kulima au kuweka kitu chochote kwenye maji kitakachoingilia mtiririko wa asili wa maji katika chanzo cha maji;
(h) anaweka kitu chochote kwenye maji taka ambacho kinaweza kuathiri mtu yeyote au kuharibu mfumo wa tiba ya maji taka;
(i) analima kilimo cha matuta yanayosababisha maji kutuama ndani ya eneo la katikati ya mji,
(j) anajenga choo chini ya umbali wa mita sitini kutoka kisimani, bwawani, mtoni, au chanzo kingine cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;
(k) anatoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu, yenye kinyesi kutoka kwenye choo, bafu au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote ulio wazi;
(l) anatupa taka au kuelekeza mtu mwingine atupe taka mahali popote pasiporuhusiwa na Halmashauri;
(m) anauza chakula katika eneo ambalo halijasajiliwa kwa ajili ya shughuli hiyo;
(n) anazika maiti katika eneo ambalo halikuainishwa kwa shughuli hiyo;
(o) kwa makusudi, anashindwa kulipa ada ya taka kwa miezi miwili mfululizo;
(p) anatembeza vyakula mitaani bila kibali cha Halmashauri;
(q) anachezesha michezo au kuonesha michezo au burudani katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
(r) anaegesha gari bovu na kuliacha kando ya barabara, kichochoro au eneo la wazi ambalo halijaidhinishwa kwa shughuli za gereji kwa zaidi ya siku moja;

(s) analima ndani ya chanzo cha maji;
(t) hana pipa la taka lenye mfuniko katika eneo la biashara;
(u) hana choo au ana choo kibovu au kilichojaa; au
(v) hana chombo maalumu cha kukusanyia taka ndani ya gari la abiria.

Adhabu

**16**. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au vyote.

Kufifilisha kosa

**17.** Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10)*

ADA YA UZOAJI TAKA

| NA | AINA YA BIASHARA/MAENEO YA UZALISHAJI TAKA | MIJI YA KIBIASHARA<br>(ENEO LOTE LA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO) | MAKAO MAKUU YA KATA TOFAUTI NA MIJI YA KIBIASHARA ADA KWA MWEZI (SHILINGI) | MAKAO MAKUU YA VIJIJI TOFAUTI NA MAKAO MAKUU YA KATA, ADA KWA MWEZI (SHILINGI) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makazi ya Familia | 1,000 | 800 | 500 |
| 2. | Nyumba ya kulala wageni | 10,000 | 8,000 | 5,000 |
| 3. | Ofisi ya umma na binafsi | 2,000 | 1,000 | 500 |
| 4. | Taasisi ya kifedha | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 5. | Benki za kibiashara | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 6. | Duka la kubadilisha Fedha | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| VYAKULA NA VINYWAJI | | | | |
| 7. | Hotel | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 8. | Mgahawa | 5,000 | 1,000 | 500 |
| 9. | mgahawa (vitafunwa na vinywaji baridi) | 8,000 | 3,000 | 1,500 |
| 10. | Duka la vyakula na vinywaji | 8,000 | 3,000 | 1,500 |
| 11. | Baa (pombe, vinywaji baridi na vikali) | 10,000 | 4,000 | 2,000 |
| 12. | Baa na mgahawa | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 13. | Baa na nyumba ya kulala wageni | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 14. | Baa, nyumba ya kulala wageni na ukumbi wa starehe | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 15. | Baa na ukumbi wa starehe | 5,000 | 3,000 | 2,000 |
| 16. | Baa na klabu ya usiku | 10,000 | 5,000 | 1,000 |
| 17. | Bucha la nyama na samaki wabichi | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| | | | | |

*Tangazo la Serikali Na.505 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| DUKA JUMLA NA REJEREJA | | | | |
| 18. | Vyakula na bidhaa mchanganyiko | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 19. | Nguo | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 20. | Vifaa ya umeme | 5,000 | 2,000 | 500 |
| 21. | Vifaa vya ujenzi | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 22. | Vitabu, shajara na zawadi | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 23. | Sonara na vipodozi | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 24. | Vinywaji na pombe kali | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 25. | Vipuri | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| 26. | vifaa | 8,000 | 3,000 | 1,000 |
| KARAKANA NA VIWANDA | | | | |
| 27. | Fundi selemala na mashine ya mbao | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 28. | Karakana ya chuma | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 29. | Karakana ya magari | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 30. | Sonara na uhunzi wa vito | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 31. | Shughuli za vioo | 10.000 | 5,000 | 2,000 |
| 32. | Mchapishaji | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 33. | Viwanda vikubwa (kwa tani moja ya taka) | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 34. | Viwanda vidogo (kwa tani moja ya taka) | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| BIASHARA NDOGO NDOGO | | | | |
| 35. | Fundi cherehени | 10,000 | 5,000 | 2,000 |
| 36. | Fundi viatu | 500 | - | - |
| 37. | Saluni ya nywele (kike na kiume | 2,000 | 1,000 | 5,00 |
| 38. | Dobi | 2,000 | 1,000 | 500 |
| 39. | Genge/meza ya biashara | - | - | - |
| 40. | Watengeneza juice/barafu na bisi | 1,000 | 500 | - |
| 41. | Wachoma chipsi na nyama choma | 5,000 | 3,000 | 2,000 |
| 42. | Waosha magari, pikipiki na bajaji | 2,000 | 1,000 | 500 |
| 43. | Mashine za kusaga/kukoboa nafaka | 5,000 | 3,000 | 2,000 |
| 44. | Waziba pancha mitaani | 1,000 | 500 | - |
| 45. | Wauza mitumba ndani ya soko | 500 | - | - |
| 46. | Wauza mitumba nje ya soko | 3,000 | 2,000 | 1,000 |
| 47. | Mama/Baba lishe | 2,000 | 1,000 | 500 |

*Tangazo la Serikali Na.505 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| HUDUMA ZA AFYA | | | | |
| 48. | Duka la dawa baridi za binadamu | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 49. | Maabara binafsi ya vipimo | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 50. | Zahanati binafsi | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 51. | Hospitali binafsi | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 52. | Kituo cha afya binafsi | 15,000 | 8,000 | 5,000 |
| 53. | Madawa asili | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| TAASISI ZA MAFUNZO | | | | |
| 54. | Shule binafsi | 20,000 | 10,000 | 5,000 |
| 55. | Chuo binafsi | 30,000 | 15,000 | 8,000 |
| VITUO VYA MAFUTA | | | | |
| 56. | Kituo kikubwa | 50,000 | 30,000 | 15,000 |
| 57. | Kituo kidogo | 30,000 | 15,000 | 8,000 |
| 58. | Kituo cha mafuta ya Taa | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 59. | Kituo cha Kuuzia Gesi | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 60. | Kibanda cha kuuzia mkaa | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| MENGINEYO | | | | |
| 61. | Duka la simu, kampuni ya simu na manara wa simu | 10,000 | 5,000 | 3,000 |
| 62. | Taka za uvunjaji wa nyumba kwa tani | 20,000 | 10,000 | 5,000 |

______________

JEDWALI LA PILI

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi;……………………………………nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya……………………………………..…….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;…..…. Mwaka;……..… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya….. ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe;…....... ya Mwezi;………… Mwaka;…………..
Jina;………………………………..…………………….
Saini;………………………..……………………………
MBELE YANGU :
Jina;…………………………..……..……………………
Cheo;…………………………………………………..…….
Saini;…………………………………………………………
Tarehe;……………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imebandikwa katika hizi Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kufuatia Azimio la kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kilichofanyika tarehe 12/5/2023 na kushuhudiwa,

Lakiri imebandikwa mbele ya:-

IKUPA H. MWASYOGE,
*Mkurungenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Lushoto*

MATHEW MBARUKU,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Lushoto*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*,